KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na *Nina Atcheson Meneja ya Mitaala ya SS na Huduma Binafsi - GC*

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

JUMA LA PILI: APRILI 17 – APRILI 23, 2020

NJOO, TUPUMZIKE KIDOGO

Asubuhi moja njema, nilitambua kuwa nyumba ilikuwa imetulia sana, na binti yangu wa miaka mitatu alikuwa anakosekana. Kaka zake walikuwa wanacheza pamoja, lakini yeye alikuwa haonekani po pote. Nilimwita, nikijiuliza kwamba alikuwa wapi. "Tahlia, uko wapi?" Sauti yangu ilitoa mwangwi uliosikika nyumba nzima, lakini ni ukimya ulioitikia. Nilipita kwenye vyumva mbalimbali, bila kuona dalili za kuwepo kwake.

Hatimaye, nilisikia sauti ndogo. "Mama..." Kichwa chake kidogo kikiwa kimejitokeza nyuma ya kiti changu chekundu. "Angalia," alikuwa ameshika kitabu chetu cha ibada, akiwa amefungua ukurasa wenye picha ya Yesu na malaika zake wakishuka duniani. "Anakuja leo mama?" Aliuliza, huku akionesha kupititia dirisha lililokuwa karibu naye.

Moyo wangu uliyeyuka nilipogundua kuwa alikuwa amekaa pale, akisubiri Yesu aje *leo*. Badala yake katika haraka zangu za asubuhi, nilikuwa ninaandaa kifungua kinywa, nikiosha vyombo na kupokea simu. Uharaka wa mambo haya 'muhimu' ulikuwa umenivuruga kabisa hata nisitoe muda wo wote kwa Yesu asubuhi ile. Mungu hangeongea kwa uwazi zaidi ya vile alivyoongea kupitia kwa Tahlia kwa nafasi ile. Ni kama alikuwa anasema, *Punguza mwendo na unitazame asubuhii hii. Na ninakuja haraka!...*

Leo, miaka mingi baadaye, ningali nikiyasikia maneno ya Mungu kwangu. "Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo" (Marko 6:31). Anatualika kusimama, katikati ya haraka zinazotutia wazimu kutuzunguka, ili tuwe pamoja naye. Sio kwa muda mfupi hapa na pale au kwa ajili ya kutimiza wajibu tu, bali kwa muda mzuri, kwani tunataka kutumia wakati pamoja na Mrejeshaji wa Roho Zetu.

Sasa hivi, wengi wetu tunajikuta tupo mahali ambapo tumetengwa kwenye nyumba zetu kutokana na janga la kiulimwengu. Kwa maana halisi, tumelazimishwa kutulia kwa muda toka kwenye haraka zetu za kawaida za maisha. Maisha yetu yamebadilika msimu huu. Je! Tunapumzika ndani yake katika "mahali pasipo na watu"? Je! Tunaisikiliza sauti yake tulivu na nyororo (1 Wafalme 19:12), inayotuita kutembea karibu pamoja na yeye (Yohana 15:9)? Je! Tunajitenga pembeni ili kumjua Yeye zaidi, au tunaijaza nafasi tulivu kwa kelele au mambo mengine yanayotuvuruga?

Ninakumbuka, nilipokuwa mtoto nilikuwa naimba wimbo uliokuwa na maneno haya: *"Muda pamoja na Yeye ni muda uliotumika vema. Atakuwa Faraja yako na Kiongozi wako. Muda pamoja na Yeye ni muda uliotumika vema. Daima atakuwa kando yako."* Kujenga uhusiano wetu na Mungu kwa kutumia muda pamoja na mfariji na kiongozi wetu, ni jambo la muhimu sana katika nyakati hizi tulizomo kwa sasa.

Muda wa utulivu/muda bora (Badala ya muda mwingi au mrefu) ndio jambo la muhimi zaidi

Ni jambo gani unaweza kufanya ili kuboresha muda wako wa kuwa pamoja na Mungu katika juma hili? Hebu zingatia mawazo yafuatayo:

- Mwombe Mungu akupatie shauku kubwa ya kutumia muda pamoja naye.
- Bibilia haikukusudiwa iwe ngumu kujifunza. Ni Neno la Mungu lililo hai, na anasubiri kuzungumza na wewe kupitia neno hilo.
- Njoo kwa unyenyekevu na kuomba kabla hujasoma Biblia yako, ukimwomba Mungu akupe ujumbe mahsusi unaohitaji kuusikia.
- Unaweza kuhitaji kuchukua fungu moja au sehemu ndogo ya Maandiko kila siku. Zingatia: Mungu anazungumza nini na mimi kupitia fungu hili? Ninawezaje kumtia moyo mtu fulani leo kwa ujumbe huu?

Mungu anatusubiri kwa uvumilivu tuutumie muda pamoja na Yeye kila siku (Ufu. 3:20). Je! Utasubiri kwa matarajio, kama alivyofanya Tahlia, ukitamani kuja kwake?

Mswali ya Moyoni: Ni kikwazo gani kikuu kinachokuzuia usitumie muda wa utulivu pamoja na Mungu? Je" Kuna vikwazo ambavyo unaweza kumwomba Mungu akusaidie kuviondoa ili kuondoa vurugu fulani?

Changamoto Hai ya Mohoni: Yawezekana Mungu anasubiri kutenda kupitia mambo magumu yanayotuzunguka ili atusaidie kutambua uhitaji wetu mkubwa kwake kabla hajarudi. Anatupatia fursa ya pekee kwa ajili yetu ili tupumzike kidogo ndani yake. Je! Utaitikia mwaliko wake? Hebu tudai ahadi za Yohana 15:4, 5; Isaya 26:2, 3 na Marko 6:33 tunapotafuta pumziko na uhakikisho ndani yake.

"Wale wanaompokea Yesu kupitia Neno lake, na kuzisalimisha roho zao katika ulinzi wake, maisha yao kwenye utaratibu wake, watapata amani na utulivu… Maisha yetu yanaweza kuonekana yamekanganyika; lakini kadiri tunavyojitoa kwa Mwalimu Mtendakazi mwenye hekima, atatoa kielelezo cha maisha na tabia itakayokuwa kwa ajili ya utukufu wake mwenyewe. " (Desire of Ages, uk. 331)

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili

- Ellen White, *Education*, chapter 20, "Bible Teaching and Study"
- Nina Atcheson, *As Light Lingers: Basking in the Word of God*
- Audiobook: *As Light Lingers: Basking in the Word of God* (To stream a weekly free chapter go to: www.aslightlingers.com)

SIKU YA 22 - Aprili 17, 2020

Taarifa ya Sifa! Bila kujali janga la ulimwengu mzima la COVID-19, Kanisa la Waadventista wa Sabato, linaendelea kusonga mbele katika utume. Na zinaanzishwa njia nyingi za kiubunifu na zenye kuwafikia watu wengi zaidi kuliko tulizozoea. Tumsifu Bwana!

MAMBO YA KUOMBEA
(Mch. Ted N.C. Wilson)

- Omba kwa ajili ya washiriki wa kanisa na wale wanaohuzunika kwa vifo vya hivi karibuni vya wapendwa wao kwa COVID-19. Ombea amani na faraja mioyoni mwao. Omba kwa ajili ya uponyaji kwa wale ambao wanaendelea kupambana na Coronavirus.

- Ombea washiriki wa kanisa waweze kuzipokea kwa vitendo kanuni za mtindo wa maisha yenye afya ziitwazo: NEWSTART (neno la ufupisho wa: Lishe, Mazoezi, Maji, Mwanga wa Jua, Kiasi, Hewa , Pumziko, na Imani kwa Mungu). Ni kanuni za maisha ya afya yenye ulinganifu.

- Omba kwamba ili sisi kama kanisa tuendelee kutafuta njia za kushiriki na wengine ujumbe wa afya, sambamba na Ujumbe wa Malaika Watatu, ambao ndio utume wetu wa mwisho kwa ulimwengu pamoja na hitaji letu la kuomba kwa ajili ya Mvua ya Masika ya Roho Mtakatifu, tunapoendelea kujiandaa kwa ajili ya kuja kwa Kristo mara ya pili.
- Omba kwamba katika shauku yetu ya kutafuta njia za ubunifu za kuwashuhudia wengine, tusisahau msisitizo wetu mkuu juu ya Kristo, Neno lake, Haki yake, Huduma yake ya Patakatifu, na uwezo wake wa kuokoa katika pambano kuu.

- Ombea mikutano itakayofanyika kwa njia ya mtandao ikiandaliwa na Televisheni ya *It is Written*, iitwayo: “Hope Awakens” inayozinduliwa leo duniani kote kitaifa. Tembelea: https://www.discoverhopeawakens.com). Omba kwamba watu wengi waweze kutazama na kupata uzoefu wa mfululizo wa mikutano hii kuliko ambavyo wangeweza kushiriki mikutano mubashara iliyoahirishwa kule Indianapolis.

SIKU YA 23 - Aprili 18, 2020

KULINDWA NA NENO

“Umtwike Bwana mzigo wako naye atakutegemeza, Hatamwacha mwenye haki aondoshwe milele.” (Zab. 55:22)

“Watendakazi wenzangu, hebu usiruhusu ujasiri wako kushindwa. Mungu anaithibitisha imani yako. Mkristo daima anaye msaidizi imara katika Bwana. Unapofikia mahali pa kutulia kidogo katika jitihada zako za thati kwa sababu huwezi kupata msaada unaohitajika, utue mzigo wako kwa Bwana. Kubali kuuacha pale, ukiwa na hakika kwamba Yeye aliyeahidi ni mwaminifu. Mambo ya Nini na Kwa vipi kuhusu Mungu anavyosaidia hatuyajui; bali tunajua neno moja tu, Mungu hatawaangusha wale wanaoweka matumaini yao kwake. Atakapokuwa amewathibitisha watendakazi wake kikamilifu, atawaleta mbele wakiwa wametakaswa kama dhahabu iliyosafishwa kwa moto.” Ellen White, Letter 66, June 26, 1901.

Maswali ya Moyoni: Unahisi ni kwa njia gani Mungu anaikuza na kuithibitisha imani yako? Ni ahadi gani za Biblia unazozipenda ambazo huwa unazidai unapokabiliana na shida? Kama changamoto ya moyoni juma hili, kwa nini usitafute fungu jipya la Biblia linalotia moyo na ulikariri. Kisha shiriki na mtu fulani mwenye kuhitaji kutiwa moyo.

Taarifa ya Sifa: Tunamsifu Bwana kwamba makadirio ya awali ya vifo vya COVID-19 katika nchi ya Marekani yanapungua kiasi fulani. Janga pia linaendelea kupungua katika baadi ya nchi za Ulaya na matumaini yanaonekana mbele.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea wataalamu wa afya walio mstari wa mbele wanaoendelea kupambana na janaga hili. Ombea usalama wa afya zao dhidi ya COVID-19, na usalama wao kimwili dhidi ya watu walio mitaani wanaodhani kwamba watendakazi wa afya wameathirika na Coronavirus.

- Omba kwamba kuwe na uwiano kati ya kuufungia ulimwengu wote ndani ya nyumba na kufungua uchumi na shughuli kwa wakati unaofaa – kabla uchumi na biashara hazijaharibiwa kabisa.

- Omba kwa ajili ya taasisi nyingi, na biashara ndogo zinazopambana na upungufu wa kifedha kama matokeo ya kufungiwa ndani. Omba kwamba watu waweze kutafuta njia za kuzinusuru biashara ndogo ndogo zisididimie.

- Ombea wanawake na watoto walio katika hali ya hatari na wanaohitaji msaada. Omba kwa ajili ya njia za kuwafikia wenye mazingira magumu na walio dhaifu katika jamii yako.

- Omba kwa ajili ya wale wanaofanya kazi kwenye mabenki, maduka,vituo vya mafuta, na biashara zingine muhimu. Omba kwamba walindwe wasipate Coronavirus wanapoendelea kushughulika na watu wengi wanaowaendea kwa ajili ya huduma,

SIKU YA 24 - Aprili 19, 2020

KATIKA KICHO CHA NENO LAKE

“Wakuu wameniudhi bure, Ila moyo wangu unayahofia maneno yako. Naifurahia ahadi yako, Kama apataye mateka mengi.” (Zab. 119:161-162)

“Biblia ni sauti ya Mungu inayozungumza kwetu kwa uhakika sawa na ambavyo tungeisikia kwa masikio yetu. Kama tungetambua hilo, ni kwa kicho kiasi gani tungelifungua Neno la Mungu na ni kwa bidii kiasi gani tungeyatafuta mausia yake. Kusoma na kutafakari Maandiko kungezingatiwa kama ni kumsikiliza Yeye Asiye na mwisho” *A Call to Stand Apart*, p. 69

Maswali ya Moyoni: Je! Umewahi kusoma fungu katika Biblia na kujifikiria, “Fungu hili lilikuwa kwa ajili yangu! Mungu alijuaje hitaji langu leo?” Unapoendelea na siku yako leo, fikiria juu ya sababu zote zinazokufanya uweze kufurahi kwa ajili ya Neno la Mungu. Kwa hakika, kwa nini usiorodheshe sababu zinazokufanya uwe na shukrani kwa ajili ya Neno la Mungu. Anza na, “Ninalipenda neno la Mungu kwa sababu....(jaza). Kama unashindwa kufikiria mambo hayo soma Zab. 119.

Taarifa ya Sifa: Tunamshukuru Mungu kwamba Kanisa la Waadventista wa Sabato katika nchi ya Guatemala limetafuta njia ya kusambaza vikapu vya chakula vyenye mchele, maharage, nafaka, mafuta, chumvi, na sukari kwa maelfu ya washirki wa kanisa wanaoathirika kwa ajili ya karantini. Huu ni ushahidi kwamba washiriki wa kanisa wanatafuta kubeba mizigo ya wengine.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea Afrika wanapoendelea kupambana na janga la Coronavirus. Ombea washiriki wanaopambana na uhaba wa huduma za afya. Ombea kwamba maambukizi na vifo yasiwe kama inavyokadiriwa.

- Ombea maelfu ya makundi ya watu ulimwenguni, 69% ya watu wote ulimwenguni, ambao hawajasikia kwa wazi habari za Yesu, Ombea zipatikane njia zilizoboreshwa ili kuyafikia katika kipindi hiki cha zahama.

- Ombea roho ya toba na unyenyekevu kwa ajili yetu kuhusu nyakati ambazo hatukuwa waaminifu kwa Mungu katika maisha yetu na ushuhuda.

- Ombea ongezeko kubwa la washiriki wa kanisa watakaomtumikia Mungu kwa kuwapenda wengine na kushiriki kwa vitendo ukweli wa Biblia na wengine, ikijumuisha wale waliotokea kwenye dini zingine.

- Ombea wakulima wanaohangaika kupanda au kuvuna mazao bila msaada wa kawaida wa wafanyakazi, ambao wamezuiliwa kusafiri.

SIKU YA 25 - Aprili 20, 2020

KUFURAHI KATIKA NENO

“Maneno yako yalionekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu; maana nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana, Mungu wa majeshi.” (Jer. 15:16)

“Hakuna kitu kilicho kusudiwa kuimarisha akili kuliko kujifunza Maandiko. Hakuna kitabu kingine chenye nguvu ya kuinua mawazo, kutia uhai katika uwezo wa akili, kama ukweli mpana na wenye kuleta heshima wa Biblia. Kama neno la Mungu lingejifunzwa inavyotakiwa, watu wangekuwa na upana wa akili, tabia yenye heshima, na uthabiti wa nia, vitu ambavyo vinaonekana mara chache nyakati hizi.” *Christ Ed.*, p. 58

Maswali ya Moyoni: Katika siku za hivi karibuni, ni jambo gani kwa namna ya pekee lilikupa furaha katika kujifunza kwako Neno? Kwa nini usitenge muda wa kumshirikisha mtu fulani juu ya jambo hilo?

Taarifa ya Sifa: Hospitali za Jiji la New York zilitarajiwa kufurika wagonjwa, wakikosa vitanda na mashine za kupumulia. Lakini, ingawa wamekuwa wakijaa sana, bado kuna nafasi kwenye mahospitali, na Bwana asifiwe, hawajapungukiwa mashine za kupumulia. Hili ni jibu kwa maombi!

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea wanaofanya kazi za usalama, kama vile maofisa wa polisi na wengine. Kadiri ukosefu wa usalama wa kiraia unavyozidi kuongezeka katika baadhi ya maeneo duniani, omba ulinzi kwa ajili ya wanaume na wanawake hawa.

- Ombea Divisheni yenye nchi zilizokuwa chini ya Sovieti kama vile Urusi na Siberia. Omba kwamba pamoja na ugumu wa kushuhudia, njia mpya zibuniwe za kuwafikia watu.

- Ombea nchi zinazoumia zilizo kwenye dirisha la 10/40. Omba Mungu atume watu watakaoshuhudia upendo wake. Ombea kwamba serikali ziruhusu watu kwenda mashambani kulima vyakula. Mamilioni ya watu katika India wamezuiwa na hawaruhusiwi kutoka nje ya nyumba zao, kwa hiyo wana njaa.

- Ombea viongozi wa kanisa wapewe hekima wanapohitaji kufanya maamuzi ya muhimu kwa ajili ya siku za usoni kama matokeo ya zahama ya kiuchumi tunayokabiliana nayo sasa.

- Ombea hekima na jinsi ya kupunguza matumizi bila kuumiza watu na kudumisha kazi za lazima na utume wa kanisa kusonga mbele.

SIKU YA 26 - Aprili 21, 2020

KUONGOZWA NA NENO

“Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!” Mika 6:8

“Tunaishi katika kipindi makini cha historia ya ulimwengu huu. Mustakabali wa makutano wanaotetemeka unakaribia kuamuliwa. Ustawi wetu wenyewe wa siku za usoni na pia wokovu wa watu wengine unategemea njia tunayoifuata sasa. Tunahitaji kuongozwa na Roho wa ukweli. Kila mfuasi wa Kristo inampasa kuomba kwa bidii: “Bwana, unataka nifanye nini?” Inatupasa tujinyenyekeze mbele za Bwana, kwa kufunga, kuomba na kutafakari sana Neno lake, na hasa matukio ya hukumu. Wakati huu inatupasa kutafuta uzoefu wa kina na ulio hai wa mambo ya Mungu. Hatuna muda wa kupoteza. Matukio ya umuhimu mkubwa yanatukia kutuzunguka; tupo kwenye uwanja wa uchawi wa Shetani. Wajumbe wa Mungu, Tusilale; adui huotea kwa karibu, akiwa tayari wakati wo wote, utakapozembea na kusinzia, akurukie na kukufanya uwe mawindo yake.” *The Call to Stand Apart*, p. 69

Maswali ya Moyoni: Unapokabiliana na uamuzi wenye changamoto, unatafuta wapi hekima na ushauri? Ni kweli kwamba, kwa wingi wa washauri huja wokovu (Mithali 11:14). Lakini, nje ya hekima ya wale tunaowapenda au wale tunaowaheshimu, ni kanuni gani tunaweza kuzipata katika Neno la Mungu za namna ya kufanya maamuzi? (Angalia Mithali 3:5, 6, Mitthali 14:12, Mathayo 6:33, Yeremia 33:3)

Taarifa ya Sifa: Juma lililopita, Divisheni ya Kusini mwa Amerika, kama ilivyofanya kwa miaka 50 iliyopita, iliwasilisha “Juma Takatifu,” programu ya uinjilisti ya divisheni nzima. Kwa kawaida vikundi vidogo hukutana majumbani na makanisani, lakini kwa sababu ya Coronavirus, divisheni inatoa programu yote kwa mtandao ikiwa na mahudhurio mengi zaidi. Mada ni *“Love Written with Blood”* (yaani, Pendo Limeandikwa kwa Damu), na limejumuisha programu za watoto, matineja, na watu wazima. Tunamshukuru Mungu kwa njia za kiubunifu ambazo viongozi wa kanisa wanazitumia kusaidia kushuhudia upendo wa Mungu.

MAMBO YA KUOMBEA

- Omba kwamba wale waliogundua upendo wa Yesu kwa mara ya kwanza, kwenye programu za Divisheni ya Kusini mwa Amerika, waweze kukuza uhusiano wa kudumu pamoja na Yesu ambao utaendelea kuwa mzuri kadiri muda unavyopita.

- Omba kwamba wote tutumie muda wa ziada tulionao nyumbani kujifunza kwa kina Neno la Mungu na kuwafundisha watoto wetu namna ya kujifunza na kulipenda Neno la Mungu.

- Ombea watu wa Mungu wadumu kuwa waaminifu katika kutoa zaka na sadaka hata katikati ya changamoto za sasa za kiuchumi.

- Ombea wale wanaoshindwa kulipa bili na kupata chakula kwa sababu ya changamoto za kiuchumi zilizoletwa na janga la COVID-19. Omba kwamba Mungu azidi kuwafadhili watoto wake na ili kuwe na ushuhuda mwingi wa uaminifu wa Mungu siku zijazo.

- Ombea kazi ya Mungu kule Lebanoni ili Mungu aruhusu upatikanaji mahitaji ya kifedha na asaidie utume wa kanisa kusonga mbele.

SIKU YA 27 - Aprili 22, 2020

KUJAZWA NA NENO

“Neno Moja nimelitaka kwa Bwana, Nalo ndilo nitakalolitafuta, Nikae nyumbani mwa Bwana Siku zote za maisha yangu, Niutazame uzuri wa Bwana, Na kutafakari hekaluni mwake.” (Ps. 27:4)

“Ninaye Mwokozi aliyefufuka. Katika Yeye ninatumaini, na hataniacha niaibike. Ninashinda katika jina lake. Yeye ni haki yangu na taji ya furaha yangu. Hebu ye yote hapa asihisi kuwa hali yake haina matumaini, kwani haiko hivyo. Unaweza kuona kuwa ni mwenye dhambi na mchafu, lakini ni kwa sababu hiyo unamhitaji Mwokozi. Kama una dhambi za kuungama, usipoteze muda. Nyakati hizi ni za thamani. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote (1 John 1:9) Wale wenye njaa na kiu ya haki watajazwa, kwani Yesu ameahidi hilo. Mwokozi wa thamani! Amenyoosha mikono yake ili kutupokea, na moyo wake mkuu wa upendo unasubiri kutubariki.” *Counsels for the Church,* p. 48

Maswali ya Moyoni: Ni jambo gani una shauku nalo zaidi? Ni nini kilio chako cha kina moyoni? Inawezekana hujawahi kulifikiria hilo hivi karibuni. Yawezekana ndio kwanza unajaribu kupambana. Au inawezekana unalifikiria hilo muda wote. Leo tumia muda kidogo kufikiria ni wapi unaweza kuipata furaha yako na utimilifu mkuu. Unapofanya hilo, tafakari Zab. 27:4, na umwombe Mungu akupe moyo wenye njaa ya kweli ya kuwa mbele zake.

Taarifa ya Sifa: Video ya Coronavirus kwa ajili ya wasiosikia imetengenezwa na Divisheni ya Magharibi mwa Afrika kule Abijan, Cote d’Ivoire, ikiwa na taarifa za muhimu kuhusu COVID-19. Tunashukuru kwa ajili ya masomo hayo mapya yaliyotengenezwa ili kuyafikia makundi yote ya watu.

MAMBO YA KUOMBEA

- Omba Mungu awalinde watoto wake kule Korea ya Kaskazini, Korea ya Kusini, Japani na China. Omba kwamba macho yote, hata ya maofisa wa serikali, yageukie mbinguni wanapotambua dalili za nyakati, na kwamba Yesu anakuja haraka.

- Waombee wale walio sehemu ya huduma za wenye Mahitaji Maalum. Ombea wale wanaofanya kazi miongoni mwa wasiosikia, walemavu wa viungo, nawengine wenye mahitaji maalumu. Waombee wenye ukoma ili wasisahauliwe au kupuuzwa wakati huu.

- Omba kwamba tunapotambua ukaribu wa kuja kwa Yesu wote tuweze kuwa na muda wa kumtafuta kwa mioyo yetu na kuchimba kwa kina Neno lake. Omba tuweze kuushika ukweli maridadi na wa kina wa vitabu vya Biblia vya Danieli na Ufunuo.

- Ombea wamishenari waliokwama kwenye vituo vyao vya kazi katika maeneo mbali mbali kote duniani. Omba wapate mahitaji yao ya kimwili na ulinzi.

- Ombea wale waliopona kutokana na Coronavirus ili wapate nguvu na miili yao ijengwe upya. Omba ili wapate nguvu tena na kurudia maisha ya kawaida.

SIKU YA 28 - Aprili 23, 2020

KUTIWA NGUVU KWA NJIA YA NENO

“Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Heb. 4:12

“Oh, ili watu wamche Mungu! Oh, ili wampende Bwana. Oh, ili wajumbe wa Mungu waweze kuhisi mzigo kwa ajili ya roho zinazopotea! Ndipo hawatahutubia tu; lakini watakuwa na nguvu ya Mungu inayotia uhai roho, na mioyo yao itawaka kwa moto wa upendo wa Mungu. Kutoka kwenye udhaifu watakuwa na nguvu; kwani watakuwa watendaji wa neno. Watasikia sauti ya Yesu: “Tazama nipo pamoja nanyi siku zote.” Yesu atakuwa mwalimu wao; na neno wanalohudumu litakwenda haraka na litakuwa na nguvu, na lenye ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili. *Testimonies to Ministers and GW*, p. 143

Maswali ya Moyoni: Unapotafakari Waebrania 4:12 unalionaje Neno la Mungu likiuchoma moyo wako mwenyewe? Je! Umewahi kushawishika na jambo fulani ulilosoma katika neno la Mungu hivi karibuni? Je! Umafanyia kazi yaliyokugusa, au ulitupa pembeni misukumo ya Roho Mtakatifu? Mshirikishe mtu fulani mawazo yako. Kisha omba kwamba sisi kama watu tusisikilize na kulipenda Neno tu, bali tutafute kuishi sawa na Neno.

Taarifa ya Sifa: Tunamsifu Mungu kwa imani kwa ajili yya roho ambazo atazileta kama mwitikio wa watu kutokana na tukio la uinjilisti la “Hope Awakens” Tunamsifu kwa ajili ya watu ambao tayari wameamua kumpokea Yesu.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea wale walio katikati ya zahama ya COVID-19, ambao ama wanahangaika wenyewe, au wanao wapendwa wao wanaosumbuliwa na ugonjwa.

- Ombea amani kwa washiriki wa kanisa ulimwenguni kote wenye hofu na wanaoogopa, au wanaohisi upweke.

- Ombea mamilioni ya watu wanaotaabika katika nchi za Mashariki ya Kati, kama vile Iran, Aghanistan, na Pakistan. Omba kwamba katikati ya zahama hii Mungu afungue mioyo mingi iupokee ukweli.

- Ombea mipango mipya inayoandaliwa kwa ajili ya Sesheni ya Konferensi Kuu iliyopangwa upya kufanyika Mei 20-25, 2021 kule Indianapolis. Ombea sesheni ijazwe na mipango ya kiroho na utume na kwamba Roho Mtakatifu awe na udhibiti kamili.
- Ombea umwagwaji wa Mvua ya Masika kwa kanisa, ili tuweze kumaliza kazi kisha twende nyumbani.